

**BODI YA USAJILI WA  
WABUNIFU MAJENGO NA  
WAKADIRIAJI MAJENZI**



**MASHINDANO YA INSHA  
MWAKA 2018**

**SHIRIKI UJIPATIE ZAWADI  
NONO**

**TAARIFA ZA USHINDANI NA  
NAMNA YA KUMPATA MSHINDI**

**1.0 Utangulizi:**

Bodi ni Taasisi ya Serikali inayosimamia sheria Na.4 ya mwaka 2010. Mojawapo ya shughuli zake ni kusajili na kuratibu mienendo ya wataalamu katika fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi na Taaluma zinazoshabiana nazo hapa nchini.

Kwa kuwa huduma hizi hutolewa kwa jamii, Bodi imeona ni vyema mwaka huu kuwashirikisha tena wanafunzi wa shule za Sekondari wa **Kidato cha Pili** kuandika Insha kueleza jinsi wanavyozielewa fani za Ubunifu Majengo (Architecture) na Ukadiriaji Majenzi (Quantity Surveying).

**2.0 Sifa za Kushiriki:**

Wanaoruhusiwa kushiriki ni wanafunzi walio katika ngazi ya **Kidato cha Pili (2) pekee na wasiozidi umri wa miaka 16.**

**3.0 Insha Inahusu Nini?**

Uwepo wa Viwanda ni miongoni mwa fursa zinazochochea maendeleo ya jamii na taifa haraka, kwa kutumia mifano fafana dhana zifuatazo;

(i) .Kiwanda ni nini?

(ii).Wataalam gani huhitajika Kwenye ujenzi wa viwanda.

(iii).Elezea nafasi ya Wabunifu Majengo(Architects) na Wakadiriaji Majenzi(Quantity Surveyors) katika kuwezesha Ujenzi wa Kiwanda.

**Lugha na Namna ya Kuandika:**

Lugha itakayotumika katika kuandika Insha ni Kiswahili. Mwandishi anaweza kuomba ushauri kutoka kwa mtu yeyote. Insha iandikwe kwa mkono, **Isipigwe Chapa** mahali popote. Maandishi yasizidi **kurasa tatu** katika karatasi nyeupe zenye ukubwa usiozidi sentimeta 21 kwa 30('A4 size').

**Angalizo:** Wanafunzi watakaonakiliana watafutiwa matokeo yao.

**4.0 Utambulisho wa Mwandishi:**

Taarifa za mwandishi zijazwe katika fomu iliyoambatanishwa na kupigwa mhuri na mkuu wa shule baada ya kuhakikisha mwanafunzi amezingatia vigezo vyote.

**5.0 Mwisho wa Kupokea Insha na Utoaji wa Matokeo:**

**Tarehe 31 Mei, 2018** ni mwisho wa kupokea Insha.

**6.0 Namna Ya Kutuma:**

Insha iwekwe kwenye bahasha na kufungwa kwa gundi. Juu ya bahasha andika anwani ifuatayo:-

**'MASHINDANO YA INSHA MWAKA 2018'**

Msajili,  
Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi,  
S. L. B. 72673,  
**DAR ES SALAAM.**

**Insha ziwasilishwe kwa njia ya Posta au kwa mkono katika ofisi za Bodi zilizopo Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, Mbeya na Arusha.**

**7.0 Namna Ya Kumpata Mshindi:**

**7.1 Vigezo Vitakavyotumika Katika Kuamua:**

Jopo la Waamuzi litachambua uelewa wa mwanafunzi kuhusu

mada, mwandiko na mambo ya utambulisho. Waamuzi wataangalia uzingatiaji wa masharti yalioainishwa kwenye tangazo.

**7.2 Mgawanyo wa Alama Zitakazotolewa Katika Kuamua:**

Alama za maamuzi zitakuwa kama ifuatavyo:- Mwandiko na urahisi wa kusomeka 5 Uelewa wa somo linalolengwa 20 Uhusiano wa kilichopo kwenye Insha na somo lenyewe 40 Matumizi ya Lugha 15 Mantiki katika mtiririko wa mawazo 20. Wastani wa ufaulu ni alama 50.

**8.0 Jopo la Waamuzi:**

Wadau waliopo katika fani ya Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi wataombwa kuamua ni nani Washindi wa Shindano hili.

**9.0 Zawadi:**

Washindi	Zawadi
Wa Kwanza Kitaifa	500,000.00
Wa Pili Kitaifa	300,000.00
Wa Tatu Kitaifa	200,000.00
Wa Nne hadi wa Kumi Kitaifa	150,000.00
Washindi wa Mikoa	100,000.00
Shule itakayotoa Mshindi wa Kitaifa	300,000.00
Shule itakayoongoza Katika Ushiriki	200,000.00
Shule Zitakazoshiriki	Cheti

Washindi watatu wa ngazi ya Kitaifa watachukua zawadi zao mahali na siku iliyopangwa na Bodi kutoa zawadi ikiwa watapenda kufanya hivyo. Bodi itagharimia usafiri na malazi kwa washindi tu.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na **Msajili** kwa anuani ifuatayo:

Msajili  
Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi  
S. L. P. 72673 Dar es Salaam  
Simu: 255 (022) 2110292, 2117546  
Nukushi: 255 (022) 2117535  
Barua pepe: info@aqrb.go.tz,  
Tovuti: [www.aqrb.go.tz](http://www.aqrb.go.tz)

**BODI YA USAJILI WA WABUNIFU MAJENGO NA WAKADIRIAJI  
MAJENZI TANZANIA**

**(Iambatanishwe Juu ya Insha)**

<b>TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI/SHULE</b>		
<b>JINA LA SHULE NA ANWANI</b>		
<b>JINA LA MWANAFUNZI</b> (Andika majina matatu)		
<b>UMRI WA MWANAFUNZI</b>		
<b>JINSIA</b> (Weka alama ya tiki ✓)	<b>MWANAUME</b>	<b>MWANAMKE</b>
<b>KIDATO/MKONDO</b>		
<b>JINA LA MZAZI /MLEZI</b>		
<b>NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI</b>		
<b>JINA LA MWALIMU MKUU</b>		
<b>NAMBA YA SIMU YA MWALIMU MKUU</b>		
<b>BARUA PEPE YA MWALIMU MKUU</b>		
<b>SAHIHI YA MWALIMU MKUU NA MHURI WA SHULE</b>	<b>SAHIHI</b>	<b>MUHURI</b>
<b>KATA SHULE ILIKO</b>		
<b>TARAFI SHULE ILIKO</b>		
<b>WILAYA NA MKOA</b>	<b>WILAYA</b>	<b>MKOA</b>